

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)

TAARIFA YA TAFTISHI/UCHUNGUZI
(INQUIRY)
(MABADILIKO YA UKUMBI WA MKUTANO)

MADA: Maombi ya Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Arusha (AUWSA) ya kutaka kurekebisha bei za huduma zake.
TAREHE: 8 Desemba 2006 siku ya Ijumaa.
MUDA: Saa 3:30 Asubuhi
WAPI: **UKUMBI WA MANISPAA ARUSHA**

Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji (*The Energy and Water Utilities Regulatory Authority (EWURA)*), imepokea maombi ya Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Arusha, (*Arusha Urban Water Supply and Sewerage Authority -AUWSA*) ya kutaka kuongeza bei za huduma zake (*tariff adjustment No. TR-W-06-007*) ya tarehe 13 November 2006.

Kulingana na sheria na taratibu za EWURA (Cap 414), na kwa mujibu wa marekebisha ya sheria hii husika, EWURA itafanya mkutano wa kupata maoni kuhusiana na taftishi/uchunguzi kutoka kwa wadau wa mwombaji ili kujua uhalali wa maombi hayo ya kurekebisha bei za huduma zake. Nakala za maombi na nyaraka za AUWSA zilizowasilishwa EWURA zinaweza kusomwa na mtu yeyote wakati wa saa za kazi kati ya saa 3 asubuhi na saa 11 jioni katika ofisi za EWURA kwa anuani iliyotajwa hapo chini.

EWURA imeandaa mkutano utakaofanyika katika ukumbi wa mikutano wa **UKUMBI WA MANISPAA ARUSHA**, siku ya **Ijumaa, tarehe 08 Desemba 2006**, kuanzia saa tatu na nusu asubuhi, ili kupata maoni ya wadau wakiwemo Baraza la wawakilishi wa watumiaji wa huduma husika (*Consumer Consultative Council -CCC*), Baraza la wawakilishi kutoka Serikalini (*Government Consultative Council-GCC*) pamoja na wadau wengine kuhusu ombi hilo la AUWSA. Wawakilishi wa

AUWSA pia wamealikwa kwenye mkutano huo ili washiriki kwenye taftishi/uchunguzi huu.

Wananchi wanaopenda kushiriki katika taftishi/uchunguzi huu pia wanaalikwa kuhudhuria mkutano huo. Wadau wengine ambao wanapenda kutoa maoni kuhusiana na taftishi/uchunguzi huu wanakaribishwa kuleta maoni yao ki-maandishi na kuyatuma kwenye anuani iliyoonyeshwa hapa chini, kabla ya saa 11 jioni tarehe 04 Desemba, 2006. **Makabrasha na nyaraka husika zinapatikana pia katika ofisi za AUWSA kwa Mkuu wa Kitengo cha Mipango na Ujenzi.**

Ni wale walijisajili tu ndio watakaopata fursa ya kuwasilisha maoni yao siku hiyo ya taftishi/uchunguzi.

Wadau wengine ambao wanapenda kutoa maoni kuhusiana na taftishi/uchunguzi huu wanakaribishwa kuleta maoni yao ki-maandishi yakiambatanishwa na kiapo. Maombi hayo yatumwe kwenye anuani iliyoonyeshwa hapa chini ndani ya siku saba, baada ya siku ya taftishi yaani kabla ya tarehe 15 Desemba, 2006.

Ufafanuzi zaidi unaweza kupatikana kwa kuandikia EWURA. Mdau yeyote anapenda kupata nakala za makabrasha atalipia gharama za kunakili na za posta.

**Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Udhhibiti wa huduma za Nishati na Maji
(EWURA), Ghorofa ya 6, Harbourview Towers (zamani JM
Mall Building), Samora Avenue, P O Box 72175
DAR ES SALAAM**